

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA SABA**

**14 APRILI, 2022**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

**KIKAO CHA SABA – TAREHE 14 APRILI, 2022**

### **I. DUA**

### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**58. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL  
MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Vifaa vya Maabara kwa Wanafunzi wa masomo ya Sayansi katika Shule za Sekondari Jimbo la Mbozi.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**59. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna athari gani za kijamii kwa Watumishi wenza kuishi mbali na Watoto wao.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**60. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA  
KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Omukajunguti ili kuruhusu ndege kubwa kutua Bukoba.

**61. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Shinyanga kama ilivyoanishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**62. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni kwa nini Serikali isiweke ulazima wa hitaji la Kisheria kuwa *Taxpayer Tax Audit* ifanyike kila Mwaka badala ya kusubiri miaka mitatu.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA  
14 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**

